



Tathmini ya riwaya teule za S.A. Mohammed katika kutetea haki za watoto

Alex Kinyua Mwirigi

Correspondence email: alexakinyua@yahoo.com

Article history

Received: June 29, 2023

Received in revised form: November 15, 2023

Accepted: November 22, 2023

Available online: <https://research.lukenyauniversity.ac.ke/>

IKISIRI

Haki za watoto ni suala ambalo limepewa uzito katika jamii mbalimbali ulimwenguni. Umoja wa kimataifa katika mwaka wa 1948, ibara ya 25 ulitambua utunzaji maalum wa mama na mtoto katika jamii. Watoto walipewa nafasi ya kuhutubia umoja huo kwa mara ya kwanza katika mwaka wa 2002 kwenye makao makuu ya umoja huu mjini Newyork. Kutokana na shinikizo za kimataifa na mashirika mbalimbali yanayotetea haki za watoto, serikali za ulimwengu zimeweka vipengele maalum za kikatiba za kulinda watoto. Nchini Kenya sheria maalum kuhusu haki za watoto ilipitishwa katika mwaka wa 2001. Sheria hii inamfafanua mtoto kama binadamu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane. Aidha sharia hii inatetea haki za watoto na kupiga marufuku unyanyasaji wowote dhidi yao. Inatoa haki kama vile elimu, afya, malezi bora, haki dhidi ya ajira ya watoto, haki ya kulindwa wakati wa vita, haki ya kulindwa dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, haki ya kucheza na kupewa nafasi ya kupumzika, utunzaji wa watoto wenye ulemavu miongoni mwa mengine. Sheria hii imeendelea kuimarishwa na kuhusisha vipengele vingine muhimu hasa baada ya

katiba mpya ya mwaka wa 2010 nchini Kenya. Haki za watoto ni suala ibuka lililopewa kipaumbele na wanajamii wote. Hatuwezi kuzungumzia haki za binadamu bila kugusia haki za watoto. Kutokana na mkabala huu, wanafasihi wengi pia wamejhusisha na maandishi mbalimbali yanayohusu haki za watoto. Makala hii inalenga kuchunguza jinsi riwaya za S. A. Mohammed zinavyoangazia haki za watoto na kuwalinda dhidi ya unyanyapaa. Mtaalamu huyu ni miongoni mwa wanariwaya wa visiwani ambao wameendelea kuacha taathira kubwa katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Said A. Mohamed ameandika riwaya nyingi katika vipindi tofauti. Kazi nyingi za Mohammed zimekuwa na maudhui mengi yaliyohusu unyanyasaji na utetezi wa haki za watoto kutokana na utafiti wetu wa awali. Riwaya zake zilizochapishwa kufikia uandishi wa makala hii ni: Asali Chungu (1977), Utengano (1980), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza Katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990), Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2004), Nyuso za Mwanamke (2010), Mhanga Nafsi Yangu (2012), Mkamandume (2013), Kamwe si Mbali Tena (2014) na Wenye Meno (2018). Utunzi wa S. A.

Mohammed unaweza kuangaliwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ni kazi zake zilizojifunga kwenye masuala ya jamii yake ambapo aliihakiki na kubainisha migogoro iliyotokota ndani. Kazi hizi zimejifunga katika ufafanuzi wa hali kama inavyobainika katika ulimwengu halisi na masuala ambayo yanaweza kudhihirika kihistoria. Riwaya zake za awamu ya kwanza ni pamoja na Asali Chungu, Utengano, Dunia Mti Mkavu, Kiza Katika Nuru na Tata za Asumini. Katika awamu ya pili anaandikia masuala ambayo yanahusu ulimwengu halisi na ulimwengu wa kiajabu ambapo mpaka wake hauwekwi bayana. Baadhi ya kazi hizi ni pamoja na Babu alipofufuka, Mkamadume, Kamwe si mbali tena na wenye meno Makala hii itajifunga katika kazi za awamu ya kwanza kwa kurejelea riwaya zake tatu mathalan: Asali Chungu, Kiza Katika Nuru na Tata za Asumini. Riwaya hizi ziliandikwa katika miongo mitatu tofauti na zinaweza kutupa taswira kamili kuhusu haki za watoto na namna jamii imekuwa ikizishughulikia katika vipindi mbalimbali vya kihistoria.

Maneno muhimu: Haki za watoto, Utanzu, Riwaya, Taswira, unyanyapaa

1.0 UTANGULIZI

Mafanikio ya mtu mzima yanachangiwa na malezi ya utotoni pamoja na mwingiliano wa mazingira na jamii yake. Makuzi na maendeleo ya mtoto yanachangiwa na wazazi, walezi, familia na mfumo mzima wa jamii. Mtazamo au mawazo ya jamii kuwahusu watoto, yaani kile kinachoweza kuelezwa kama itikadi ya jamii kuwahusu watoto ni jambo la kimsingi katika maendeleo ya jamii. (Wamitila 2008: 324). Aidha, watoto ni kiungo muhimu katika jamii na ndio tegemezi la ujenzi wa taifa lolote hivyo sharti walindwe na kutunzwa ipasavyo. (Katiba ya Kenya 2010, ibara ya 53).

Fasihi ya Kiswahili ni miongoni mwa fasihi ambazo zimechangia katika kuwasilisha masuala tofauti tofauti ya kijamii. (Sabula na Sangili, 2019). Mojawapo ya masuala ya kimsingi yanayoangaziwa ni suala la haki za watoto. Hii inatokana na sababu kuwa kuna uhusiano kati ya jamii na fasihi hivyo fasihi ni njia mojawapo ya kumulika matatizo yanayoikumba jamii yakiwemo tabia nchi, ukosefu wa chakula, udhalilishaji wa watoto na mengineyo. Kwa mujibu wa Warren na Welleck (1973), fasihi ni kielelezo cha jamii. Kwa hivyo, fasihi huwa na mshikamano mkubwa na asasi za jamii na hivyo masuala mengi ya kifasihi huwa masuala ya kijamii. Mwandishi vilevile huwa ni zao la jamii na huwa anaongozwa na hali halisi ya maisha ya wakati wake na kuzingatia katika utunzi wake. Mwengo wa makala hii basi ni kutathmini jinsi mwandishi S. A. Mohamed anavyohakiki masuala mbalimbali katika jamii yake hususan suala la ujitokezaji wa haki za watoto. Tutahoji jinsi suala la haki za watoto linavyoakisika katika riwaya teule za Asali Chungu, Kiza Katika Nuru na Tata za Asumini.

2.0 KIUNZI CHA NADHARIA

Makala hii iliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa iliyoasisiwa na Maxim Gorky (1934). Wataalam wengine wanaohusishwa na nadharia hii ni George Lukacs, Zhadnov na wengineo. Istilahi 'Uhalisia' ilitumika nchini Ufaransa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1850. Hegel (1971), alitumia istilahi hii kufafanua kazi za sanaa zilizo na wahusika ambao msukumo wao uliongozwa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Wataalam wengi wanaohusishwa na dhana hii ya uhalisia wa kijamaa, walishikilia kuwa jukumu la mtunzi ni kudhihirisha ukweli jinsi ulivyo na pia kukashifu maovu yanayotokea katika jamii. Mwandishi anastahili kuchora taswira ya jamii yake pamoja na kuwasawiri wahusika

na mandhari yanayoakisi jamii ya wakati wake.

Kutokana na kukithiri kwa ubepari katika maeneo mengi ya ulaya ambayo yalikuwa kiini cha uhalisia, maskini walitumiwa kama nyenzo ya kuzalisha mali huku faida yote ikiishia mikononi mwa mabwenyenye. Jambo hili lilizua mgogoro baina ya tabaka la chini la wachochole na tabaka la juu lililohodhi utajiri na mamlaka. Mgogoro huu hutokea kwa sababu kila mara tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Hivyo, inalazimu kuwa na mapinduzi dhidi ya njia za kuzalisha mali ambazo zinahimili unyanyasaji. Mapinduzi haya yanajenga matumaini ya kuwepo kwa jamii mpya inayoongozwa na usawa, (Eagleton, 1976). Mvutano baina ya tabaka la wanaonyonya na tabaka la wanaonyonywa ndio ulizua kuibuka kwa nadharia ya uhalisia wa kijamaa pale ambapo wanajamii walibaini kuwa matakwa ya wanajamii yanajengeka zaidi kwenye nguvu za kiuchumi na sio katika majaliwa wala fikra, (Khaemba, 1999). Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilitumika kama zana ya kuleta usawa hivyo kutatiza uhalisia wa maisha. Kutokana na uchanganuzi tulioutoa kuhusiana na nadharia ya uhalisia wa kijamaa, ifuatayo ni baadhi ya mihimili ya nadharia hii:

Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalani wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao. Ni kwa msingi huu ambapo tunahakiki riwaya tatu teule za S. A. Mohamed ambazo zinarejelea masuala ya jamii yake kama vile haki za watoto na kuwasawiri wahusika katika mazingira halisia ya kijamii.

Pamoja na kusawiri matukio kihistoria, wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. Hufanya hivi kimaksudi au bila kufahamu. La mno ni kwamba tabaka la wanyonge hujifungata masombo kujipa mamlaka ya

nguvu za kiuchumi. Katika riwaya ya Asali Chungu, wahusika kama Bwana Zuberi na Bi. Amina wanawakilisha tabaka la juu linaloendeleza dhuluma dhidi ya tabaka la chini. Vilevile, Bwana Juba wa Kiza Katika Nuru amesawiriwa kama bwenyenye anayeendeleza dhuluma dhidi ya wanyonge. Mfumo wa utawala unaowakilishwa na viongozi kama Bwana Zuberi na Bwana Juba bila shaka utawaathiri watoto wanaojipata katika familia za wazazi ama walezi wa tabaka la chini lililotawaliwa na umaskini.

Uhalisia wa kijamaa huzingatia maslahi ya makabwela. Hawa ni mafukara wa ulimwengu wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela.

Wahusika wa kimaendeleo: Hawa ni wahusika wanaonua kuipindua na kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao.

Huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamaanisha kwamba mtu atakuwa mshindi au ni mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.

Lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii.

3.0 KUMHUSU MWANDISHI SAID AHMED MOHAMED

Mohamed alizaliwa mwaka wa 1947 kisiwani Zanzibar mjini. Alijiunga na chuo cha Ualimu cha Nkurumah mjini Zanzibar mwaka wa 1966. Alianza kufundisha katika shule za msingi na secondari mnamo miaka ya 1969 – 1974. Alifundisha masomo ya Bayalojia, Hesabu, Kemia na Kiswahili. Wakati huo huo alikuwa akiandika hadithi fupi katika vituo vya BBC na Deutsche Welle; mashirika ya Uingereza na Ujerumani mtawalia. Alijiunga na kidato cha 5 na 6 ambapo alikuwa amepanga kufanya masomo ya sayansi lakini ukosefu wa vifaa vya

utekelezi ukampelekea kufanya somo la sanaa. Mwaka wa 1976 alijiunga na Chuo kikuu cha Dar es Salaam ambapo alihitimu kwa shahada ya B. A. Baadaye alihitimu shahada ya Uzamili ambapo alisomea isimu tekelezi.

Mohamed alifundisha katika idara ya Kiswahili chuoni Dar es Salaam kwa muda mfupi kabla ya kuelekea Chuo kikuu cha Leipzig Ujerumani ambapo alihitimu kwa shahada ya uzamifu mwaka wa 1985. Alisafiri nchini Kenya kufundisha Kiswahili katika Chuo kikuu cha Moi mwaka wa 1987 na baadaye katika Chuo kikuu cha Nairobi mwaka wa 1990. Baadaye alienda Ujapani na kujiunga na chuo cha masomo ya kigeni kule Osaka ambapo alipanda ngazi na kuwa profesa. Mnano 1997 alijiunga na chuo kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani hadi kustaafu kwake.

Mohamed ni mwanzuoni na mwandishi hodari ambaye amechangia katika takribani tanzu zote za fasihi andishi zikiwemo ushairi, tamthilia, hadithi fupi, riwaya, kazi za wototo na pia vitabu vya shule na vyuo. Kazi zake ni pevu zinazoenziwa sio tu katika Afrika Mashariki na Kati bali popote pale Kiswahili kinaenziwa. Hii ni kwa sababu ya ubora na wingi wa kazi zake ambazo huvutia kimtindo, kimuundo, kiwahusika na kimsuko.

3.1 UCHAMBUZI WA RIWAYA YA ASALI CHUNGU

Katika riwaya ya Asali Chungu (1977), tunasawiriwa Bwana Zuberi ambaye ni kabaila anayemiliki ardhi na pia ofisa wa utawala katika enzi ya ukoloni wa Waingereza. Sifa kuu za Zuberi ni kwamba ni fisadi asiyewajibika kazini mwake. Anatomia muda wake mwingi kuwatongoza wanawake. Bwana Zuberi ni bwana shamba dhalimu ambaye anamlazimisha mhudumu wake wa kike kulala naye. Mwandishi anadhihirisha udhalimu wa mfumo katili wa utawala

ambapo Waingereza walitawala Zanzibar kwa kushirikiana na makabaila wa Kiarabu kama Zuberi.

Katika mfumo huu wa utawala, jamii imegawika katika matabaka. Tabaka la juu ni la mabwana shamba na lile la chini la watumishi wao. Watumishi hawa ni wategemezi wa mabwana shamba, hawana haki zozote na maisha yao ni dhiki tupu. Watoto wanaozaliwa katika familia za tabaka la chini kama Dude wanaishia kukata tamaa maishani. Uk. 32, Dude anayaona maisha kama mashaka na kwake siku ya kufa inakaribia. Toka alipozaliwa, Dude alitwika masaibu ya ulimwengu na alikuwa majeruhi wa mateso, madhila na sulubu. Kwa hakika, analazimika kuacha masomo katika darasa la sita kwa sababu ya ukosefu wa karo.

Hatimaye tunaonyeshwa jinsi ambavyo tabaka la wanyonge linavyoingana kutekeleza mapinduzi ili kudai haki zao kwa nguvu. Kundi la watu lenye hamaki na silaha kali linamkabili Bwana Zuberi na familia yake. Nyumba ya Zuberi inaishia kutiwa moto ambapo yeye na mkewe Amina wanaangamia pamoja na kibaraka wao Daudi.

3.2 UCHAMBUZI WA RIWAYA YA KIZA KATIKA NURU

Riwaya hii inaanzia katika ofisi ya Bwana Juba ambapo panazuka mtafaruku kati ya bwana Juba na mwanawe Mvita. Bwana Juba ndiye mwajiri wa Mvita mbali na kuwa baba yake. Anamwachisha Mvita kazi baada ya Mvita kuanzisha harakati za kupinga dhuluma na unywonywaji wa tabaka la chini la wanyonge. Bwana Juba anawakilisha tabaka linalomiliki mamlaka na uwezo mkubwa wa kifedha.

Mvita anaendelea kuwa mpinzani wa baba yake kisiasa akishirikiana na mkewe Salma hadi pale tunapomwona Bw. Juba akimtuma Shazia kumwangamiza Mvita. Baada ya kumuu Mvita, bwana Juba anavamiwa na

mkewe Bi. Kudura na mwanawe Mbishi na kuuawa. Bi. Kudura na Salma mkewe Mvita wanatiwa gerezani lakini Bi. Kudura anajitoa uhai mle korokoroni. Salma yuko gerezani kwa sababu ya kifo cha mumewe Mvita ambacho amesingiziwa. Wafuasi wa Mvita wanamtembelea Salma gerezani na kumpa moyo kwamba angeachiliwa na wangali wafuasi wake.

3.3 UCHAMBUZI WA RIWAYA YA TATA ZA ASUMINI

Nguli katika riwaya hii ni mwanafunzi katika chuo kikuu kwa jina Asumini. Amelelewa katika mazingira magumu ambayo yanamfanya ashindwe kutangamana na wanafunzi wengine anapofika katika chuo kikuu. Mwishowe Asumini anashindwa kuendelea na masomo yake kwa kulemewa na mgogoro wa kisaikolojia. Tata zilizomo akilini mwake zinamtatiza hadi anashindwa kuchagua kati ya maisha ya kisasa na yale ya zamani aliyousiwa na wazazi wake. Katika utoto wake, Asumini alinyimwa uhuru wa kuhusiana na watoto wenzake na kulazimika kuishi maisha ya utawa.

Anapogura kutoka chuo kikuu, Asumini haendi nyumbani bali anakutana na Zaina ambaye wanaishi pamoja mpaka pale Asumini anapougua ugonjwa wa akili na kupelekwa hospitalini. Anamwandikia mchumba wake Sewa barua na kumwambia vile ulimwengu ulivyomdhulumu. Analalamikia malezi aliyopewa na wazazi wake ambayo yalimpelekea kutatizika kinafsi. Katika barua hiyo, anamshauri Sewa dhidi ya kuwalea watoto wake wa kike jinsi yeye alivyolelewa na wazazi wake.

4.0 TATHMINI YA HAKI ZA WATOTO KATIKA RIWAYA TEULE ZA S. A. MOHAMED

4.1 Haki ya kukua katika mazingira salama.

Njagi, C (2021), anasema kuwa jamii ina jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wanakulia katika mazingira yanayowahakikishia usalama dhidi ya magonjwa, njaa, vita na dhuluma nyinginezo. Kauli hii inasisitizwa katika riwaya ya Asali Chungu ambapo mwandishi anaonyesha jinsi watoto wanavyoweza kuvimba kichwa na kupotoka kutokana na tabia wanazoziona katika mazingira wanamoishi. Dude ambaye ni mwana wa Semeni na Baya binti wa Bi. Pili, ni watoto wanaojipata katika mazingira hatari. Wazazi wao ni walevi kupindukia na makahaba. Wana mazoea ya kuingia na wanaume pale nyumbani na kuwaonyesha wana wao vitimbi. Mfano mzuri ni Dude ambaye anayaona matendo ya mama yake yakitendeka waziwazi machoni pake. Mtoto huyu anavutiwa na tendo hili na kutamani sana kulijaribu. Hatimaye wale watoto wawili (Dude na Baya) wanaishia kushiriki vitimbi walivyoviona kwa wazazi wao. Wazazi hapa wakawa vielelezo wasiofaa kwa wana wao. Kwa njia hii, mwandishi anawatahadharisha wazazi dhidi ya kukipotosha kizazi cha kesho kwa kukipa mwelekeo usiofaa:

“Baya akawa mwanamke na yeye ndiye mwanamume.

Lakini wao hawakudhubutu kutenda dhahiri.

Hawakuwa na uhuru kama wazee wao.

Ilibidi waibiebie mpaka pale wazee wanapokuwa hawapo.

Hapo Baya huwa mke, na Dude huwa mume.” (Asali Chungu 37).

Baadaye watoto hawa wanaishia kuwa raia wasiotegemewa katika jamii kutokana na athari za ulezi wao. Utu uzimani tunakutana na Baya kakata tamaa maishani, lake kubwa ni ulevi kupindukia na kuuza mwili. Tunamwona Dude akishiriki mapenzi na

Amina ambaye ni mama zaidi ya rika la mama yake mzazi. Dude anapopata mke kwa jina Shemsa hatulii kabisa licha ya kupendwa sana na mkewe; anampa mimba Latifa ambaye ni dada yake mkewe tena mtoto mdogo kiumri. Hatimaye anaungama Dude kuwa kazaliwa katika mkosi, na maisha ataishi katika mkosi. Hivyo ndivyo alivyoamini. (Asali Chungu 182).

4.2 Haki ya kupendwa na kulindwa

Kila mtoto ana haki ya kupendwa na kutunzwa na wazazi wote. Haki hii inapaswa kuzingatiwa bila kuhusisha tofauti zozote zilizopo baina ya wazazi. (UNICEF, 1989). Kwenye Kiza Katika Nuru (1988), mwandishi anaonyesha matokeo ya watoto waliotelekezwa na baba yao. Licha ya Bwan Juba kuwa kiongozi mwenye mamlaka na uwezo mkubwa wa kifedha, ameiacha familia yake kuangamia katika lindi la umaskini. Vilevile ametoweka kabisa katika maisha ya watoto wake wanaomhitaji kwa ushauri pamoja na mahitaji ya kimsingi. Kudura-mama yake Mbishi alizipokea kesi za ubishi wa mtoto wake kila wakati. Mbishi aliwahasudu watoto wenzake kwa kutamani vitu vyao ambavyo hakununuliwa na baba mzazi japo alikuwa tajiri aliyenuka pesa. Hivyo maskini aliishia kupigana na wenzake.

Mwandishi anasisitiza umuhimu wa mfumo wa uongozi kuwajibika ili kukielimisha kizazi cha kesho. Vinginevyo watoto wanaopaswa kuwa shuleni huishia kujitafutia chakula kutokana na umaskini uliosababishwa na viongozi mafisadi kama Bwan Juba. Tazama:

“Tena walitokeza kundi la watoto katika kinyang’anyiro

cha vidagaa vilivyowadondoka wavuvi.

Na wengine walisafisha madamu na kugombea uronda

waliobakishiwa.” (Kiza Katika Nuru 1988: 193).

4.3 Uhuru wa kujieleza na kushirikishwa katika maamuzi

Mtoto ana majukumu ambayo anachangia katika jamii yake. Hivyo, ni muhimu kumshirikisha katika maamuzi ya kijamii husani yale yanaomlenga kwa njia moja au nyingine. Aidha, mtoto anapaswa kupatiwa uhuru wa kufurahia na kutangamana na mazingira yake. (Njagi, C. 2021). Mwandishi anashtumu utumwa wa watoto na kuhimiza umuhimu wa watoto kupewa uhuru wa kujijua, kujielewa na kutangamana na wenzao kadri wanavyokua.

Wazazi wanatahadharishwa dhidi ya kuwa wakali zaidi kwa watoto wao kama inavyoelezwa katika nukuu hii:

“Na malezi ya babaake na mamaake yakawa

malezi na kulemaza wakati mmoja.” (Tata za Asumini 1990: 19)

Asumini alinyimwa utamu na uhuru wa kukua kama watoto wenzake. Analia kwa unyonge wa kunyang’anywa uhuru wake wa kucheza michezo ya utotoni kama watoto wengine wa majirani.

Matokeo ya kulelewa huku kwa Asumini yanabainika wazi anapojipata katika mgogoro wa kisaikolojia wa kujisaka. Asumini hauelewi mwili wake, haielewi nafsi yake na hayaelewi mazingira yake. Hivyo anaingia katika motifu ya safari ngumu ya kujijua ambayo inamtatiza sana kisaikolojia. Mara si moja Asumini anaonyesha tabia za mtu aliyerukwa na akili kutokana na matatizo haya ya nafsi. Upo wakati anatoa rundo la nguo safi na chafu, mpya na kuukuu na kushikilia kuwa alitaka kuzisafisha. Mara Asumini anaitiwa polisi baada ya kumrushia kila mtu mchanga kwenye harusi. Kwenye Disco Asumini

anazua vurugu mpaka Disco linafungwa. Polisi wanamkamata kwa wiki moja mpaka daktari anapothibitisha kuwa akili za Asumini hazijatulia. Ni wazi kuwa huyu ni mhusika ambaye anatatizika sana kiakili na matatizo haya yanaweza kuangaliwa kama matokeo ya malezi yake.

4.4 Haki ya elimu

Katiba ya Kenya (2010) kipengele cha 53, inasisitiza kuwa kila mtoto ana haki ya kupata elimu na serikali sharti iweke mipangilio mwafaka ili kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata elimu hususani elimu ya msingi. Haki hii inashadidiwa na S. A. Mohamed anapositiza umuhimu wa mfumo wa uongozi kuwajibika katika kukielimisha kizazi cha kesho. Vinginevyo, watoto wanaopaswa kuwa shuleni huishia kujitafutia chakula kutokana na umaskini uliosababishwa na viongozi mafisadi kama Bwana Zuberi na Bwan Juba. Hali hii inampitikia Dude katika Asali Chungu ambapo anakabiliwa na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi akiwa mtoto mchanga. Kwa hakika analazimika kuacha masomo katika darasa la sita kwa sababu ya ukosefu wa karo.

5.0 HITIMISHO

Makala hii imeangazia ujitokezaji wa haki za watoto katika riwaya teule za Asali Chungu, Kiza Katika Nuru na Tata za Asumini. Kutokana na matokeo ya uchunguzi, imebainika kuwa S. A. Mohamed anatambua nafasi muhimu ya mtoto katika jamii ya kitaifa na kimataifa na hivyo kuisawiri katika kazi zake. Ameonyesha dhahiri kuwa matatizo yanayowakumba watoto yanapaswa kuelekezwa katika mazingira wanamokulia na zaidi katika jamii pana katika kile anachokiita mfumo wa jamii. Mwandishi anaukashifu mfumo wa jamii ambao unakosa kumwakikishia mtoto usalama wake. Hapana shaka kwamba mtunzi ametoa mchango murua kwa kuangazia mojawapo ya masuala yanayoakisika katika jamii nyingi kama

inavyofafanua nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Aidha, riwaya zilizochanganuliwa zinaweza kuangaliwa kama viwakilishi vya nyakati na enzi tofauti tofauti na zenye thamani ya kifasihi.

MAREJELEO

- Convention on the Rights of the Child. (20/11/1989). Available <https://www.unicef.org/child-rights-convention>
- Eagleton, T. (1996). *Literary Theory*. London: Blackwell Publishing.
- Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism*. London: Methuen.
- Gorky, M. (1975). *On Literature*. Washington: University of Washington Press.
- Hegel, G. (1971). *Introduction to Aesthetics*: Oxford: Clarendon.
- Human Rights Watch: *Explore Children's Rights*. (25/5/2022). Available <https://www.hrw.org/topic/children's-rights>.
- Lukacs, G. (1979). *The meaning of Contemporary Realism*: London. Merlin.
- Mohamed, S. A. (1977). *Asali Chungu*: Nairobi: Shungwaya Publishers.
- Mohamed, S. A. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (1990). *Tata Za Asumini*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Njagi, C. (2021). *Children's Right to Participation in Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijchapishwa).
- Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Shirika la Umoja wa Mataifa. (10/12/1948). Available <https://www.un.org/en/about-us/universal-declaration-of-human-rights>.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
- Warren, A. na Wellek, R. (1973). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.